



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI
ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO ANAWATANGAZIA WANAVIKUNDI FURSA YA KUOMBA MIKOPO ITOKANAYO NA ASILIMIA (10%) YA MAPATO YAKE YA NDANI. AIDHA MIKOPO HII NI KWA AJILI YA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU VYENYE VIGEZO VILIVYOAINISHWA HAPO CHINI; KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KATIKA ROBO YA KWANZA

A: MAOMBI YOTE YATAFANYIKA KWA NJIA YA MTANDAO

Kikundi kinachokusudia kuomba mkopo ni lazima kiwe na vigezo vifuatavyo;

- Kiwe kimesajiliwa kama kikundi cha wanawake, vijana au watu wenye ulemavu;
- Kiwe kinajishughulisha na ujasiriamali
- Kwa kikundi cha wanawake au vijana lazima kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia kumi na kuendelea na kwa kikundi cha watu wenye ulemavu lazima kiwe kina idadi ya wanakikundi isiyopungua watano na isiyozidi kumi;
- Lazima kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya kikundi; na
- Wanakikundi wake ni raia wa Tanzania wenye akili timamu na umri wa miaka kumi na nane na kuendelea
- Kiwe ni kikundi kisichojumuisha wajumbe wenye ajira rasmi.
- Kiwe na wanachama wanaotoka eneo moja ndani ya kata husika.

- Kiwe na mradi wa kikundi (shughuli ya pamoja)
- Kwa vikundi vya vijana, ni lazima wawe na vitambulisho vya Taifa vya NIDA/Vitambulisho vya Mpiga kura ambavyo lazima viambaishwe kwenye maombi yao ya mikopo.

B: UTATATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Kwa kikundi kilichokidhi vigezo vya hapo juu kinachokusudia kuomba mkopo kitatakiwa kujaza fomu maalum inayopatikana kwenye Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata ikiambatishwa na nakala za nyaraka zifuatazo:

- (i) Katiba ya kikundi;
- (ii) Cheti cha usajili wa kikundi;
- (iii) Muhitasari wa kikao cha kikundi unaoidhinisha uombaji wa mkopo husika
- (iv) Kwa vikundi vinavyojishughulisha na biashara, leseni ya biashara;
- (v) Taarifa ya akaunti kutoka katika benki ambayo kikundi kina akaunti;
- (vi) Barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji au Kata; na
- (vii) Wazo la biashara.
- (viii) Nakala za NIDA za kila mwanakikundi.

Namna ya kuomba tumia tovuti hii. mikopo.halmashauri.tamisemi.go.tz

KWA UFAFANUZI ZAIDI FIKA OFISI YA KATA ULIYOPO.

Imetolewa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero.


SIA L NGAO

KNY: MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MVOMERO.



Halmashauri ya Wilaya Mvomero, S.L.P. 663, Morogoro, Simu: +255232934348, Nukushi: +2552334348,

Barua pepe: ded@mvomerodc.go.tz, tovuti: www.mvomerodc.go.tz